**HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO**

**SHULE YA SEKONDARI LYAMKENA,**
**S.L.P 151 ,**
**MAKAMBAKO.**
**25/11/2020.**

Kumb Lyss/JOIN/2020/01
JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………..

**YAH:FOMU YA MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA LYAMKENA SEKONDARI 2021**

Uongozi wa shule, jumuiya pamoja na wazazi kwa ujumla tunakupongeza sana kwa kuchaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari katika Shule hii.Ni matumaini yetu kuwa utaitumia fursa hii vizuri kwa maslahi na faida yako binafsi, jamii inayokuzunguka na taifa kwa ujumla .

Wajibu wako mkubwa ni kusoma kwa bidii, kufuata sheria za shule kushiriki kikamilifu katika kazi za mikono, uzalishaji mali,kuishi kwa amani, upendo na ushirikiano baina yako na wanafunzi wenzako walimu na watumishi wengine wasio walimu ili kujipatia elimu bora na yenye tija itakayokuwezesha kuishi maisha yaliyo endelevu.Mafanikio yatapatikana endapo utakuwa mwenye kujituma na kunakoambatana na **nidhamu .**

Shule ya sekondari Lyamkena ni shule ya kutwa na ni ya mchanganyiko wa wasichana na wavulana.Inafundisha masomo ya Hisabati,Kemia,Baiolojia,Kiswahili,Uraia, Jiografia, Kiingereza, Fizikia na Historia.Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili na utatakiwa kuzungumza kiingereza muda wote utakapokuwa katika mazingira ya shule.
Shule ipo kilomita 5 kutoka ofisi ya Halmashauri ya Mji pembezoni mwa barabara kuu ya magari iendayo Njombe. Mita 168
Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** fika na mzazi/mlezi wako siku ya kufungua shule.

**HONGERA SANA NA KARIBU SANA LYAMKENA SEKONDARI**

**MTITU M.S,**
**MKUU WA SHULE.**
**0755 214 870.**

1. **VIFAA VYA SHULE**
   A. Daftari kubwa zisipungue kumi [Counter book]
   B. Mkebe [Mathematical set]
   C. Rula, kalamu za wino [peni] za kutosha na kalamu za risasi [penseli] za kutosha
   D. Mkoba nadhifu wa kubebea daftari
   E. File moja la kutunzia kumbukumbu zake binafsi kama vile mitihani
   F. File la kutunzia kumbukumbu [flat file] liletwe shuleni siku ya kufungua shule
   G. Graph paper kwa matumizi binafsi
   H. Aje na nakala ya [copy] ya cheti cha kuzaliwa

**2 SARE ZA SHULE**

**A.WAVULANA.**

i. Suruali mbili rangi nyeusi kitambaa kizito [Estimu namba moja] zingatia kushona mshono wenye maadili na isiyo ya kubana.
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vinavyotumia kiwi vyenye kisigino kifupi jozi mbili au zaidi
iv. Soksi nyeusi jozi tano au zaidi
v. Sweta mbili za rangi ya kijani jeshi zenye shingo ya V

**B. WASICHANA**

i. Suruali mbili za rangi ya kijani jeshi isiyo bana
ii. Blauzi mbili nyeupe [tazama mchoro umeambatanishwa]
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vinavyotumia kiwi kisigino kifupi jozi mbili au zaidi
iv. Soksi nyeupe jozi tano au zaidi
Hijabu ifanane na sare ya shule [nyeupe kwa waislamu]
v. Sweta mbili za rangi ya kijani jeshi zenye shingo ya V

**C. MAVAZI YA MICHEZO KWA WANAFUNZI WOTE**

vi. Raba jozi moja
vii. T-shirt moja ya rangi ya bluu
viii. Bukta moja
ix. Truck suit rangi nyeusi yenye fito nyeupe jozi moja
x. Soksi ndefu jozi moja

**3.CHAKULA CHA MCHANA.**

Ili kuboresha taaluma na afya wanafunzi wote wanatakiwa kula chakula cha mchana shuleni na ni muhimu kwa wanafunzi wote hivyo basi kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia kama vile ifuatavyo

A .Mahindi debe mbili kwa mwaka au Debe moja kwa muhula

B.Maharage debe moja kwa mwaka au Lita kumi kwa muhula [Nafaka mbovu hazitapokelewa]

C.Fedha Tshilingi elfu thelathini kwa mwaka [30,000/=] au Tshilingi 15,000/= kwa muhula fedha ziwekwe kwenye **AC. NO 60310023983 EK LYAMKENA SEKONDARI** Wasilisha risiti ya kuweka fedha bank yenye jina la mwanafunzi kwa kamati ya chakula ya wazazi siku ya kufungua shule.

**4 MENGINEYO.**

B). wasichana waje na fagio (soft grooms) na wavulana waje na mopa kwa ajili ya usafi.

NB**: HATUA KALI ZITACHUKULIWA KWA KILA MZAZI /MLEZI ATAKAYESHINDWA KUMLETA MTOTO SHULENI NA KUTOTEKELEZA MAJUKUMU YAKE IKIWA NI PAMOJA NA KUTOMPA MAHITAJI YA MSINGI MTOTO WAKE.**

**MAKAMBAKO TOWN COUNCIL**

LYAMKENA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 151,
MAKAMBAKO,
DATE……………………………………..

REF.NO.LYSS/JOIN/2021/01
THE MEDICAL OFFICIER
………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………

**REF.REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Kindly examine [name]…………………………………………………………….
To determine her/his physical and mental fitness to pursue secondary education.

i. EYESIGHT………………………………………………………………………
…
ii. HEARING………………………………………………………………………
…
iii. SPEECH…………………………………………………………………………
…
iv. Limbs……………………………………………………………………………
…
v. Leprosy…………………………………………………………………………
…
vi. Epilepsy……………………………………………………………..…………
vii. Cardiac diseases.………………………………………………………………
viii. Rheumatism……………………………………………………..……………
ix. Venereal diseases…………………………………………..……………
X Pregnancy for girls…………………………………………..……………….
Xi Any other serious diseases……………………………………………………
Xi Any disabilities……………………………………………………………………

Name of medical officer…………………………………………Signature………………………
Designation…………………………………Date………………………………
Stamp

**THE HEADMASTER**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanunuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

A. Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
B. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
C. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni.
D. Kuwahi katika kila shughuli za shule nyingine utakazopewa.
E. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
F. Kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira ya shule.
G. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
H. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
I. Kutunza mali za umma.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,Cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau bendera ya taifa.
viii. Kuwa mjamzito au kupata mimba.
ix. Kuoa au kuolewa.
x. Kutoa mimba.
xi. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au wa watu.
xii. Kukataa adhabu ka makusudi.
xiii. Kuwa na simu ya mkononi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

**MTITU S.M**

**MKUU WA SHULE.**

**SHULE YA SEKONDARI LYAMKENA**
**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

A.MWANAFUNZI

JINA LA MWANAFUNZI.............................................................................................
ANUANI.......................................................................................................................
Mimi............................................................................................................................

Nimekubali kujiunga na shule ya sekondari Lyamkena.Nimesoma kwa makini maagizo ya shule na kuyaelewa.Naahidi kuwa nitazingatia sheria /taratibu za shule kama nitakavyoelekezwa.

Sahihi.........................................................Tarehe......................................................

B.MZAZI/MLEZI
Mimi.............................................................................................................................
Mzazi/Mlezi wa.............................................................................................................

Nimesoma kwa makini maagizo ya shule na kuyaelewa.Naahidi kuwa nitazingatia. Pia kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza ,kumlea mwanangu kielimu kimwili na kiroho pia.Nitatoa michango yote iliyo halali kwa wakati.

Sahihi...........................................................Tarehe.............

# FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

## A.HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi..........................................................................................
2. Mahali ulipozaliwa..............................Tarehe ya kuzaliwa..............................
3. Dini...................................................Dhehebu.............................................
4. Shule uliyotoka...................................................................................................
5. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama vile mpira wa miguu,mpira wa pete,riadha, kuimba na kadhalika n.k.......................................................

## B.HABARI ZA WAZAZI

1. Baba yu hai.....................ndiyo/hapana, mawasiliano Simu.............................
2. Mama yu hai...................ndiyo/hapana, mawasiliano Simu.............................
3. Jina la mzazi/mlezi anayekulea..........................................................................
4. Uhusiano na mlezi...............................................................................................
5. Kazi ya mzazi au mlezi...........................Namba ya simu ya mlezi..................
6. Jina la balozi.........................................Namba yake ya simu........................
7. Mahali anapoishi mzazi /mlezi..........................................................................

Mtaa/kitongoji.......................................Kata...................................................
Sahihi ya mzazi/mlezi...........................Tarehe...............................................
Sahihi ya balozi....................................Tarehe..............................................

C.**NDUGU WENGINE WA KARIBU**

| NA | JINA | UHUSIANO | ANWANI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| **01.** | | | | |
| **02.** | | | | |
| **03.** | | | | |

## D.OFISI YA MTENDAJI WA KATA AU MWENYEKITI WA MTAA AMBAKO MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ANAISHI

1. Jina.............................................................Namba ya Simu...........................
   Mtendaji wa kata ya.........................................................................................
2. Jina la mwenyekiti wa mtaa......................................Namba ya simu.............

Jina la mtaa au kitongoji.........................................................................